TANGAZO LA SERIKALI NA. 126 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KYAMALANGE YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Kyamalange ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mipango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba.

**JEDWALI**

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye barabara kuu ya kijiji cha Katale kwenda kwenye kitovu cha kijiji cha Rubafu kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VU 64 yenye majira - nukta 370380MS, 9883004KZ; baada ya hapo mpaka unafuata gema la mwamba kwa umbali wa kilomita 1.16 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VU 164 yenye majira - nukta 370224MS, 9884157KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 2.067 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VU137 yenye majira - nukta 371543MS, 9885749KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.176 hadi kwenye ufukwe wa ziwa Victoria kwenye majira nukta 371663.9760MS, 9885887.7732KZ; baada ya hapo mpaka unafuata ukingo wa ufukwe wa

*Tangazo la Serikali na.126 (linaendelea)*

ziwa Victoria kwa kuelekea Kusini hadi kwenye makutano ya kijito kidogo cha Nyamishasha unapoingia ziwa Victoria kwenye majira - nukta 371836.1755MS, 9882407.9456KZ; baada ya hapo mpaka unafuata kijito cha Nyamishasha Kaskazini - Magharibi hadi kwenye majira - nukta 3708850.9738MS, 9882830.3916KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.49 hadi jirani na barabara kuu ya kijiji cha Katale kwenda kwenye kitovu cha kijiji cha Rubafu kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VU 64 yenye majira - nukta 370380MS, 9883004KZ hadi ulipoanzia".

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*